

## 10- Nasaha Za Mafanikio Ya Hajjum-Mabruwr

Hadiyth za Rasuli (صَلَى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) zimetaja kwamba Hajjum-Mabruwr jazaa yake ni Jannah<sup>1</sup> na kila mwenye kuhiji anatarajia malipo hayo matukufu kabisa. Lakini vipi mtu aweze kuipata Hajjum-Mabruwr? Nasaha zifuatazo zitasaidia kufanikisha hilo In Shaa Allaah.

### 1-Ikhlaasw

Weka niyyah safi kuitekeleza Hajj yako kwani ‘amali yoyote isiyokuwa kwa niyyah safi haipokelewi. Niyyah isiwe kwa ajili ya lolote jingine isipokuwa kutaka Radhi za Allaah (سبحانه وتعالى).

### 2-Kuitekeleza Kwa Kufuata Sunnah Ya Rasuli (صَلَى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ):

Muislamu anapaswa kutekeleza ‘Ibaadah zake zote kwa kufuata mafunzo ya Rasuli (صَلَى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ). Baadhi ya watu hutekeleza ‘ibaadah na taratibu kinyume na amri yake aliposema:

((خُذُوا عَنِّي مَنَاسِكَكُمْ))  
((Chukueni kutoka kwangu manaasik zenu))<sup>2</sup>

Atakayefanya hivyo, atakuwa amepoteza juhud zake na mali yake na hatofaulu katika kufikia lengo la Hajj na kupata thawabu zake kwa sababu Rasuli (صَلَى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) ameonya:

((مَنْ أَحْدَثَ فِي أَمْرِنَا هَذَا مَا لَيْسَ فِيهِ فَهُوَ رَدٌّ))  
((Atakayezusha katika jambo yetu hili lisilokuwa (katika Dini)  
yetu basi litarudishwa))<sup>3</sup>

### 3-Subira

---

<sup>1</sup> Tazama Mlango wa Fadhila Za Hajj.

<sup>2</sup> Muslim na wengineo

<sup>3</sup> Al-Bukhaariy na Muslim

Jifunze na jitayarische kuwa na subira ya hali ya juu kwa sababu huko ni mkusanyiko wa watu wasiopunguka milioni tatu! Na sehemu kadhaa inabidi wakusanyike watu wote kwa wakati mmoja. Kwa hivyo kunakuwa na msongamano mkubwa wa watu. La kutahadhari zaidi ni kwamba huenda mtu akasukumwa na aliye nyuma yake apate kusogea mbele. Kitendo hicho ni cha kumkasirisha mtu, na hapo ndipo inapohitajika subira ya hali ya juu ili usije kugombana naye au yejote mwengine atakayekufanyia dhulma ya aina yoyote, kwani kutokuvumilia kutasababisha ukose kutimiza kauli ya Allaah (سبحانه وتعالى) Aliyokataza mabishano, magomvi n.k.

#### **4-Kujiepusha Na Shirki**

Shirki ni jambo linalobatilisha ‘amali za mwana Aadam kwa hivyo itakuwa ni khasara kubwa mno kupoteza muda wako, ghamama, tabu na mashaka kukosa malipo ya Hajj. Anaonya Allaah (سبحانه وتعالى):

﴿إِنَّ أَشْرَكَتْ لَيَخْبَطَنَ عَمَلُكَ وَلَتَكُونَنَ مِنَ الْخَسِيرِينَ ﴾

((“Ukifanya shirki bila shaka zitaporomoka ‘amali zako na bila shaka utakuwa mionganini mwa waliookhasirika”))<sup>4</sup>

Ni muhimu kabisa kuhakikisha kwamba humshirikishi Allaah (سبحانه وتعالى) na jambo lolote katika ‘ibaadah zako. Mionganini mwa yanayotendeka ya shirki ni kuomba du’aa kwa kumuita asiyekuwa Allaah (سبحانه وتعالى) amtakabalie, au kugusa kuta za Al-Ka’bah, za Masjid au kaburi la Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) na kujipangusa mwilini. Au kuelekea makaburi kuomba du’aa au kuitakidi jambo fulani au kitu fulani kina manufaa nawe.

#### **5-Kuhifadhi ‘Amali Kutokana Na Maasi Na Dhulma**

Muislamu anapaswa kujiepusha na aina zote za maasi; uongo, kutotazama wanawake na wanawake kutokutazama wanaume. Wanaume kutokuwagusa wanawake makusudi kubishana katika biashara, kujiepusha na mijadala na upuuzi wowote, kupiga soga n.k.

---

<sup>4</sup> Az-Zumar (39: 65).

Tahadhari kumdhulumu mtu; kumsukuma, kumuumiza kwa vyovoyote, kumpiga, kumtusi, kumvunja heshima yake kwa njia yoyote, kumuibia mali yake, kughushi, kumsengenya, kumkejeli, istihizai, kumcheka n.k. Hayo yote ni dhulma inayoharibu 'amali za mtu. Rasuli (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) ameonya aliposema:

**((Je, mnajua muflis?))** Wakasema [watu]: "Muflis kwetu sisi ni yule mionganini mwetu asiyekuwa na dirhamu [pesa] wala vyenye kumnufaisha yeye hapa duniani." Akasema ((صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)) **Hakika muflis katika Ummah wangu ni yule atakayekuja Siku ya Qiyaamah na Swalaah, Swawm na Zakaah, lakini amemtusi huyu, amemsingizia huyu mwingine kuwa amezini, amekula mali ya huyu, amemwaga damu ya mwingine na kumpiga mwengine. Thawabu zake zitapatiwa huyu na yule mpaka zimalizike. Na zinapokwisha basi madhambi ya hao [aliowadhlumu] atabandikwa nayo, kisha aingizwe Motoni)).<sup>5</sup>**

## 6-Jizidishie Elimu

Kuwa karibu na watu wema na wenye elimu ili uweze kufaidika nao katika mafunzo yanayohusu Hajj na mengineyo yatakayokufaa Aakhirah. Hudhuria darsa Misikitini unufaikie kwa elimu. Wenye elimu waandae darsa watakapokuwa Minaa, darsa za mafunzo mbali mbali yakiwemo Fiqh ya Hajj, kuamrishana mema na kukatazana maovu.

## 7-Kumdhukuru Allaah (سبحانه وتعالى)

Fanya jitihada kumdhukuru Allaah (سبحانه وتعالى) wakati wote kwa kuomba maghfirah na tawbah, kuomba du'aa, kuleta tasbiyh, tahmiyd, tahliyl, takbiyr, kusoma Qur-aan, kumswalia Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), n.k.

## 8-'Ibaadah Za Naafilah n.k.

Jitahidi ujichumie thawabu maradufu kwa kufanya 'ibaadah ziada za Sunnah; kuswali kila unapopata fursa ukiwa Masjid Al-Haraam na Masjid

---

<sup>5</sup> Muslim.

An-Nabawiy kwani fadhila zake ni maradufu.<sup>6</sup> Swalaah ya Adhw-dhwuhaa, Swalaah zilizo Muakkadah na zisizo Muakkadah, Swalatul-Witr, Tahajjud, kumdhukuru Allaah (سبحانه وتعالى) baada ya Swalaatul-Fajr mpaka jua lichomoze kisha uswali rakaa mbili ambayo thawabu zake ni kama za Hajj na ‘Umrah. Ukiweko muda mrefu huko funga Swawm za Sunnah, toa swadaqah na kutenda kila aina ya wema kwa wenzako.

---

<sup>6</sup> Tazama Mlango wa “Fadhila Za Hajj Na ‘Umrah.”